# Uwamsho

*Mt. Yohana 4:13-14, "Yesu akamjibu akamwambia, kila anywaye maji haya ataona kiu tena; walakini yeyote atakayekunywa maji nitakayompa mimi hataona kiu milele. Bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji yakibubujika uzima wa milele"*

Hebu tuangalie kile nabii wa Mungu alichosema juu ya hilo: Chemichemi ya maji yaliyo hai ……..Tumeona ni nini chemichem ya maji yaliyo hai. Tumeona birika la maji ni nini. Sasa, ni nini chemichemi ya maji yaliyohai? " Ni kisima cha chemchem (inayobubujika juu). Kisima cha chemchem, " ni nini hiyo? Ndugu Branham?" Ni kisima ambacho kila siku kinabubujika kutoka chini na kusukuma maji yake juu. Kila mara kinabadilisha, kujiwezesha chenyewe, kila siku ni mapya na masafi, kisima cha chemchemi, chimbuko la maji yaliyo hai. Haikufa na kusimama; ni maji yaliyohai. Kinabadilika kila mara, kikileta kitu kipya wakati wote. Kikiwa kinaendelea, kutoka katika chimbuko lake. Inatoa nguvu zake kutoka mahali pake, ambapo ni …..patulivu pakibubujika chimbuko la maji yaliyohai yarushwayo juu, yanayojisafisha yenyewe. Ni masafi, yasiyochanganyika, maji masafi. Kinajiwezesha chenyewe; huna haja ya kungojea mvua hujaza tariki lake. Kila mara kinabubujika juu, kinatoa maji yake bure; Huna haja ya kupampu, au kuzunguusha, au kupindisha au kujiunga nacho. Ni chemchem ya maji yaliyohai.

Unajua, chukua haya mabirika ya zamani, inabidi uzunguushe na kuzunguusha na kuzunguusha hiyo, na kupampu na kila kitu ili kupata maji yote yaliyosimama kuja juu, lakini chemchem ya maji yaliyohai inayatoa bure bila kupampu, kujiunga au kitu chochote kile (Yeremia 2:13)

Oh, nafurahi kwa ajili ya chemchem hiyo (Zaburi 36:9) Ndiyo, Bwana hayahitaji kichujio juu yake ili kutoa wadudu nje, kwa maana yanatoka ndani sana katika mwamba ambako hakuna wadudu – kule haihitaji tambara la Elimu lining'inie juu yake (Hiyo ni kweli). Taratibu fulani za kidunia zilizoundwa na wanadamu, hekima ya kidhehebu ya kwenda mbele ya mtu anayeangalia akili za watu na akuangalie kama unaweza kuhubiri au la. Haina moja ya matambara haya machafu yakining'inia juu yake. Ingelisukuma nje mara tu unapoliweka pale. Huwezi kufanya hivyo. Hivyo kisima kinabubujika wakati wote. Kama utaweka moja ya



hayo matambara juu yake, italitupilia mbali upande mmoja au mwingine. Haina muda wa matambara ya kidhehebu juu yake.

Huhitaji chujio, huhitaji kuchuja, hakuna kupampu, hakuna kusukuma wala chochote kile. Kipo pale, kinabubujika juu. Hakitegemei mazingira ya mvua kukijaza. Mvua ni uwamsho. Mahali ambapo ile chemchem…………hiyo ni pale kwenye chemchem ya uzima, ulipo mzoga ndipo tai wanakusanyika.

Huhitaji kuupampu uamsho; huhitaji kupampu kitu chochote jambo pekee upaswalo kufanya ni kuja kwenye kijito (chemchem) siku zote imejaa vizuri, maji mazuri (fresh) na hayana mwisho. Yanaendelea kububujika tu.

Huhitaji kwenda kwenye birika na kusema. "vema kama itanyesha na kutiririka kwenye ghala, 'vema tutapata kitu fulani cha kunywa" Jamani, Jamani. Siyo hii, kile kisima cha chemchem kinabubujika maji mazuri na baridi wakati wote. Unaweza ukajitegemea. Huhitaji kusema. "Vema, nitaenda katika kisima kile cha zamani. Tumezoea kunywa kutoka pale, lakini haijanyesha katika muda mrefu. Nakuambia, kinaweza kuwa kimekauka.

Hivyo ndivyo ilivyo kwenye taratibu hizi zilizofanywa na watu unaweza kuingia ndani, kama unacho kitu kikubwa kinachoendelea, kitu kikubwa (a big kaboo) na kuuza kitu fulani, michezo ya bunko na karamu maorofani chini, kila kitu, unaweza ukaona nyumba iliyojaa; lakini unaenda wapi, mahali penye chemchem inayobubujika hapo kila wakati, watu wako pale wakijipatia kinywaji cha baridi cha maji; unaweza ukakitegemea hicho. Unasema. " hawajapata uamsho kwa miaka kumi". Kama unaishi karibu na hiyo chemchemi, unao uamsho wa kila siku unaoendelea.

Hivyo ndivyo ilivyo kama unaishi kwenye chemchem hiyo ya maji yaliyohai.

Kama nisemavyo, inatoa maji bure. Huna haja ya kuweka matambara juu yake – ili kujua tambara fulani la elimu – kabla hujamtuma kwenda kuhubiri na kuona kwamba anasema maneno yake kwa usahihi, anayatamka vema, kama anatumia majina ya vitu na vitu badala (pronouns) na kadhalika, na sifa. Wengi wao hawajui mambo haya ni nini. Lakini yeye anaishi penye chemchem sawa ile ile tu.

Haihitaji kutegemea mvua za mazingira yake zinyeshe ili kukijaza au uamsho kwa mazingira yale; haihitaji kufanya hivyo,

Kwa maana nguvu zake na usafi wake ulio ndani yake. Hapo ndipo mahali penye Neno, nguvu zake zenyewe. Kama mtu anaweza kulipokea hilo moyoni mwake, hilo linao usafi wake lenyewe, nguvu zake. Liko hasa ndani ya Neno lenyewe linachomoza kuleta uzima (Yohana7:37-38).

Tunachohitaji leo sio vingi vya kimw[illegible]ivyo tunavyo. Hatuhitaji makanisa makubwa; hatuhitaji makusanyiko maku[illegible] Hatuhitaji vingi vya maredioni – na televisheni. Hatuhitaji vitu vingi ya hivyo. Lakini tunachohitaji leo ili kuwa wakiroho, ni ambaye anaweza kujinyenyekesha mwenyewe mbele za Mungu hata kama hawana hela, na wataomba mpaka ile Roho iliyo ndani yao itaridhishwa na uzuri wa Mungu na uamsho utendeke ndani ya mioyo na hilo litabadili mtazamo wao na mazingira waishio ndani yake.

Sasa, sikiliza kwa karibu sasa. Sasa, tunaona kuwa kutakuwa na vita na matetesi ya vita. Na sasa tunauona mtini ukichipua, na miti mingineyo yote inachanua, wamethodist, wabaptist, wapresbyterian na wote wanachipua, uamsho mkuu ukiendelea. Sasa, ninaamini kuwa Mungu anamkusanya Bibi Arusi kwa saa ile ya mwisho, wateule oh jamani.

Sasa, hiyo ndiyo maana leo ule uamsho tunaopaswa kumpata…………tuna uamsho wa kidhehebu; hatujapata kitu halisi cha kuchochea. Hapana, hapana, hapana. Hapana, Bwana. Usifikiri tumepata uamsho hatujapata oh, wamepata mamilioni na mamilioni na mamilioni ya wanachama wa Kanisa, lakini sio. Hakuna uamsho popote. Hapana, hapana.

Bibi Arusi hajapata uamsho bado. Unaona? Hatujawa na uamsho pale, hapana udhihirisho wa Mungu wa kumchochea Bibi Arusi bado. Unaona? tunautazamia huo. Utachukuwa zile ngurumo saba zisizojulikana ili kumuamsha yeye tena. Atatuma hilo. Ameahidi hilo.

Ndugu Braham aliulizwa swali, je, Zile ngurumo saba ambazo ni sawa na siri saba zimekwisha kufunuliwa? Je, zilifunuliwa katika zile muhuri saba ila bado – ila bado hazijajulikana kwetu kama ngurumo?

La, zilifunuliwa katika zile muhuri saba; hivyo ndivyo zile ngurumo zilivyokuwa. Ilibidi zifunue……………Zile Ngurumo saba zilitoa sauti zao na hakuna yoyote angetambua ilikuwa nini………Yohana alijua zilikuwa nini, lakini yeye alikatazwa kuandika habari zake. Yeye alisema; bali yule malaika wa saba, katika siku za kupiga baragumu yake, zile siri saba za zile Nguruma saba zitafunuliwa". Na yule malaika wa saba ndiye mjumbe wa ule wakati wa saba wa Kanisa.



Wakati mmoja nikiwa pwani ya bahari nilitazama upepo ukivuma, na ulikuwa unatikisa vema. Haikuwa pwani ya bahari; ilikuwa juu kule kwenye ziwa la Michigan. Nilisimama pale nikiangal[illegible]imbi yalivyokuwa yanakuja, na oh, lile ziwa lilikuwa linaruka, au yale maj[illegible]wa yanaruka, na mitumbwi ikitikiswa. Nami nikawaza, " Kwa nini, lile ziwa lina uamsho". Hivyo hasa linaruka na kutikisa, kwa nini? Kuna upepo wenye nguvu unavuma kuja chini juu yake. Vema nikawaza, "Vema unajua nini? Hakuna hata tone moja la maji lililoongezeka ndani ukilinganisha na lilipokuwa limetulia kimya kabisa". Hakuna maji zaidi na ndani yake, limetibuliwa tu vema, ni kitu gani limelifanya kutibuka hivyo? "unajua maji yanapotibuliwa yanafanya nini? yanaosha takataka zote nje pembeni ya ziwa.

Hicho ndicho tunachohitaji kuoshwa kutokuamini kutoka nje, pembeni, kuliruhusu Neno la Mungu lichukue nafasi ya kwanza. Hicho ndicho tunachohitaji, uamsho wa kuosha kutoamini kutoka nje, na wadudu wote (kunguni) na ushirikina na mambo, yatoke na kuona kuwa Mungu bado ni Mungu, Hivyo ndivyo hasa kusudi la uamsho(Matayo 12:38-42; Waebr 13:8).

Tunawezaje kuwa na uamsho wakati tumefungwa? Tumemfunga Roho Mtakatifu na vyama vyetu na kanuni zetu, na hatuwezi kuwa na uamsho wa Roho Mtakatifu. Amen Ninajua hilo la moto linachoma na hali ya hewa, lakini ni kweli. Tunawezaje kuwa na uamsho wa Roho Mtakatifu wakati mmefungwa na kukata tamaa?

"Kuwa na hali ya utauwa", Biblia ilisema wangekuwa. Hali ya utauwa, lakini walikana nguvu zake" Nguvu za nini? Nguvu za vyama? Nguvu za dunia? Nguvu za kanisa? Nguvu za Roho Mtakatifu. Hapo ndipo mahali pa siri ndani ya kanisa. Na kanisa linapotaka wahubiri wasomi, na majengo makubwa, na vitu vya kuonekana, badala ya mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu, ni afadhali wawe kwenye utume tena. Amen kweli utawezaje kuwa na uamsho wa Roho Mtakatifu, na watu wanajaribu kuuzima na kuufunga na huku wanauogopa huo? Hapo ndipo shida ilipo. Nafikiri huu ni wakati ambao kamwe hatupaswi kuiacha Roho ya uamsho ife. Tunapaswa tuendelee na uamsho, siku zote tufufushwe. Paulo alisema anapaswa afe kila siku ili Kristo aweze kuishi. Na kamwe hatupaswi kuacha uamsho ufe ndani yetu (1kor 15:31).

Lakini kuhusu kurudi nyuma, kumbuka, unarudi nyuma kila siku. Hakuna njia kwa wewe kuzuia hilo lisitokee. Vema Lakini unarudi nyuma machoni pa watu katika kanisa, lakini siyo mbele za Mungu……….unaona? unarudi nyuma katika Kristo, lakini siyo hivyo mbele za Mungu. Kwa sababu kama umetenda dhambi kweli, umepotea. Lakini kila mara wewe unaanguka. Paulo ilipasa afe kila siku. Hiyo ni

kweli? Ilipasa afe kila siku, atubu kila siku, na anatubu tu wakati wote unaona? Na kama Paulo alipaswa kufanya hivyo, hata mimi yanipasa nifanye vivyo pia. Si hata wewe? Hiyo ni sawa.

Sasa kama kuna mtu yoyote aliye na mitambo kwa uamsho, ni ndugu yetu mzuri, billy Graham. Lakini mitambo ni mizuri, lakini mitambo haiwezi kufanya kazi; inachukua nguvu za kuendesha. Unawezaje ukajenga gari, na kuweka viti vizuri ndani yake, na Pistoni nzuri, na likithibitishwa na sayansi vile liwezavyo kufanya; lakini mpaka nguvu za kuendesha ziwe pale, litakuwa ni kitu kizuri kilichokufa.

Hivyo katika uamsho wa Wesley, moja ya uamsho wetu uliopita kabla ya huu wetu wa Kipentekoste, hakuna hata mmoja aliyejua ni nini kilichoanzisha ule uamsho. Ilikuwa ni kundi la watu tu.

Rafiki yetu, Billy Graham, atawakusanya wapresbyterian, na walutheri na wapentekoste, na kila kitu pamoja, unaenda kwenye mji, na hapo atakuwa na kusanyiko kubwa la maelfu pamoja, na thelathini elfu watampokea Kristo katika mioyo yao kwa wiki mbili; ukirudi baada ya wiki mbili nyingine hutakuta hata mmoja unaona? Hiyo ni mitambo.

Lakini mwachie Mungu katika Neema yake mwenyewe azungumze (nitwit) na mtu mdogo asiyechochote; na acha Roho wake ashuke katika mji na watu hawataweza kwenda kazini, wanawake hawataweza kuosha vyombo, watumishi hawataweza kutandika vitanda, watapiga kelele na kulia mikono yao ikiwa juu hewani. Huo ni uamsho; ulio katika mapenzi ya Mungu. Ilisemekana wakati mmoja kuwa waheshimiwa kutoka Kanisani (Amerika) walienda kwenye uamsho wa Wesley ili kuelewa, au kujua yote kwa jinsi ya nje yaliyokuwa yanafanyika kwenye uamsho katika uamsho wa Wesley. Na waliposhuka kwenye meli na kofia zao, na ukosi wa duara; akaja polisi mwanaume barabarani, akitembea na kuzungusha rungu yake kwa nguvu, huku akipiga winja, wakamwambia, wewe mtu mzuri, unaweza kutuambia uamsho wa Wesley uko api?"

"Akasema, ndiyo ndugu zangu; hapo mlipo mmesimama katikati ya uamsho wa Wesley. Akasema, "mnaelewa, mimi ndiye uamsho wa Wesley" akasema, " kwa sababu uamsho wa Wesley uko ndani yangu"

Huo ni kwa uwezo wa Mungu. Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo, na Yeye peke yake anayo haki ya kutuma uamsho. Siyo afanyavyo, na Yeye peke yake anayo haki ya kutuma uamsho. Siyo kuweka nguvu za nje pamoja, Ni kumuomba Mungu atume nguvu za kuendeshea.



Sasa, karibuni tumeshuhudia moja ya uamsho mkuu sana, ninaamini. Ambao dunia imewahi kushuhudia katika miaka kumi, kumi na tano Lakini, sasa, katika miaka ya mwisho ya karibuni umetulia sasa. Huoni ile shauku iliyokuwa ndani ya watu.

Nakumbuka usiku mmoja kule Vandalia, ilinoisi. Niliingia katika mkutano, na hata sijakaa hata zaidi ya dakika tano katika mkutano na hakukuwa na mtu mgonjwa mahali pale pote. Viti vya matairi vilisogezwa na kurundikana rundo, vipofu walikuwa wanaona, na viziwi na mabubu walikuwa wanasema, na ilikuwa ni kitu rahisi tu, ni ……Roho wa Bwana alikuwa yupo, na yeye akaliponya tu kundi lote. Sasa, hapo ndipo unapoweza kufanya jambo fulani, wakati uamsho unaendelea.

Lakini acha moto wa uamsho ufe chini, hapo ni kwa shida sana……..watu bado ni wakristo, lakini (hawakufufushwa) au kuhuishwa katika Roho ule uwepo mkuu wa mazingira unaofanya vitu. Ni kama kwenye ofisi ya mhunzi afuaye vyuma; lazima chuma kiwe cha moto kabla hujaenda kukipiga katika Anvil. Kama hufanyi hivyo, kamwe hutaweza kukinyoosha. Hiyo ndiyo inayohitajika ili kupata uamsho, Kila mmoja awe katika joto la Roho Mtakatifu atakayeleta nguvu za Mungu katika kuufanya uamsho uendelee. Halafu kuna mikutano ya maombi inayoendelea mchana na usiku kila dakika kila mahali.

Pale ndipo hapo vipofu wanaona, viziwi wanasikia. Na huduma usiku wa leo iko mamia ya maili mbele ya hilo, lakini moto wa uamsho umekwisha zimika chini. Ndugu Branham aliulizwa tena: Imekuwaje siku hizi tunazoishi, unapokuwa mwaminio anayefuata ujumbe au mjumbe wa siku hizi, huku haionekani kama unaweza kuomba kama vile ungependa kuomba?

Hilo ni swali zuri. Naamini Ndugu, Dada, yeyote uliyeuliza, ni kwa sababu ya hali za wakati huu. Ufufuo tayari umekwisha ufufuo umedumu kwa miaka kama kumi na mitano, na haukuwa kamwe hapo nyuma umedumu kwa zaidi ya miaka inayozidi mitatu. Naamini imepokea ufufuo wake wa mwisho. Pia naamini hiyo ndiyo sababu hamwezi kuomba na kujisikia katika Roho kama mlivyokuwa mkijisikia. Ni kwa sababu mioto ya ufufuo imezimika.

Ninaona katika mikutano yetu na kadhalika ya wanaume wafanya Biashara, "Kunakuja mbele yetu, Halleluya, uamsho mkuu".

Msidanganyike "yeye amekwishakuja, na wakamtendea sawa na yote aliyoandaliwa" (matayo 17:12) Lakini wanafikiria kwamba kuna uamsho. Je unatokea? Hapana!umeshatokea umekuja umekwisha. Angalia, Huu ni wakati wa kuzitengeneza taa, wakati wa kutoka na kuingia. Bali wao wamngojeao Bwana

watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu wala hawatazimia.
(Isaya 40:31; Matayo 25:1-7).

Hili ni kwa ajili ya kanisa, mwili ule wa Kristo, ambao tunajaribu kuuongoza katika mawazo ya kilindi na malengo makuu, tukiamini kuwa kule kuja kwa Bwana Yesu kukaribu. Tunaamini hivyo zaidi.

Ni miaka ishirini karibu zaidi kuliko nilipokuja shreverport kwa mara ya kwanza oh, mengi yametokea tangu wakati huo. Sasa, tunaangalia mbele kule kuja kwa Bwana katika kizazi chetu siangalii uamsho katika kizazi chetu siangalii uamsho katika kizazi chetu; ninaangalia kule kuja kwa Bwana katika kizazi chetu.

Hiyo ndiyo sababu kila kizazi kina uamsho wao, nafasi katika Neno la Mungu. Oh, Mungu mwenyeenzi siku ya hukumu…….kundi la John Wesley litainuka, na hawa wamethodist wa leo waliokakamaa watajibu kwa yote. Luther atainuka. Na wakatoliki watainuka na nyuma kule Ireneus, Martin, Polycarp, na wote, na watasimama katika hukumu kwa kulichanganya Neno la Mungu na kanuni hili kundi la walutheri waliofuata uamsho wa walutheri watajibu jambo hilo. Lile kundi la wabaptisti walimfuata. uamsho wa John /smith watafanya jambo hilo. Alexander kampbell’s atafanya jambo hilo hilo. Na wapentekoste watafanya jambo hilo. Ule uamsho wa kwanza, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka, aliwaita watu, na Mungu akijaribu kulichukuwa Neno lake kwao, na wakaunda vyama, na wakakaa juu pake, na kuunda madhehebu na wakafa palepale.

Angalia; Lakini uone hili, yule Bibi Arusi wa kiroho anapoanza kuwa na uamsho, wakati anapokuja na kujiweka sawa na Neno la Mungu, angalia tena, jinsi maandiko, wakati ule utakuwepo ujumbe wa kumwinua tena yule bibi arusi, kumwinua yule mwanamke mteule kwa maana kama dunia …..Shetani mdanganyifu, aliyemdanganya yule Bibi Arusi wa kwanza kutenda dhambi kinyume na Mungu kwa kutoliamini Neno lake…….

Lakini sasa, lione tena lile Kanisa la kiroho, vile vile kundi la watu “ Lililoitwa litoke” Wateule katika kila uamsho wakati wa Martin Luther; ilitokea vilevile wakati wa matengenezo lilitokea jambo lilelile wakati wa John Wesley. Ilitokea jambo lilelile wakati wa Pentecoste mwanzoni ilipoanza. Waliwadondosha waliwaacha wanawake wale kule nyuma ikiwa ni sawa na Neno na halafu wakaliacha na kwenda mbali. Pale anaenda tena kule nyuma kwenye machafuko; lakini wakati watu wako tayari kukaa sawa na neno, uko ujumbe unakuja na wanakaa kwenye mstari wake.



Luther alikuwa mjumbe siku moja wa kuhesabiwa haki kwa Imani; na kanisa likakubaliana na huo baadhi yao wengineo wote waliobaki waliendelea hivyohivyo. Wesley akaja na utakaso; kanisa likakubaliana na huo. Pentekoste ilikuja na kurudishwa kwa karama; kanisa likakubaliana na huo, wateule wa siku ile na baada ya hapo ikapita wakarudi kwenda kwenye madhehebu na wakakubaliana na wote waliobaki, wote kuelekea huko nyuma kwenye mstari huo.

Lakini sasa angalia wakati watu wakianza kujaribu kusimama sawa na Neno, hapo unakuja ujumbe mpya kutoka kwenye Neno la Mungu ukiwaendea watu moja kwa moja, na iliifanya ujumbe huo uwe sawa wakati wote. Yote yatakuwa katika Mungu tunahitaji hilo. Ni saa ngapi ndugu? Ni saa ngapi mhuduma? Unaiona saa unayoishi ndani yake? Unaweza kuyaelewa? Unaiona hiyo?

Kila mahali sasa hakuna uamsho. Kila mmoja analalamika, wahudumu wanalia. Nilikuwa ninasoma moja ya magazeti muhimu maarufu ambayo yanakuja hapo kanisani, gazeti zuri sana. Na ninamjua mhariri, na ninawajua hao watu. Ni watu wacha Mungu, wazuri sana, Ndugu na Dada Moore, wa (“Herald of His Coming”) mbiu ya kule kuja kwake; moja ya magazeti mazuri sana yaliyopo, “mbiu ya kule kuja kwake”. Lakini hawachapi kitu chochote isipokuwa liwe ni “funga,omba,funga,omba. Piga baragumu pata…..”wangapi wanalisoma hilo? Mnajua, mnaliona hilo wakati wote “funga, omba,funga,omba! “ Hicho ndicho tu unachosikia funga, omba. Tutapata mapambazuko makuu ya siku (Nuru kuu). Kuna jambo kuu linaenda kutokea. Watu wote ombeni,ombeni,ombeni. Hatujachelewa bado”

Kwa nini wanafanya hivyo? Kwa nini wanafanya hivyo? Wanataka uamsho mkuu. Wanalia, wakiamini kutakuwa na uamsho. Ni watu wazuri kwa nini iko hivyo? Wamefanya nini? Hawakutambua ule uamsho wa Bibi Arusi unaona? kwa kuwa ni wakristo wanasikia ule msukumo wa saa lakini hawakutambua kile kimefanyika. Hilo ndilo linawafanya wasikie hivyo wnajua jambo fulani linapaswa litokee; lakini wanaangalia hilo kuwa liko mbali sana mbeleni, wakati tayari linatokea miongoni mwao.

Sasa hebu niseme hiki hapa. Siamini kwamba Mungu anaita wale wa kanisa la uongo watubu (ufunuo 3:19) katika mstari huu anazungumza na wateule wake. Wanayo yapasayo kutubiwa, pia wengi wa watoto wake bado wako kwenye makanisa haya ya uongo. Ni wale wanaozungumziwa katika Waefeso 15:14, “Amka wewe ulalaye katika wafu na Kristo atakuangaza Nuru yake”.

Kulala siyo kuwa umekufa. Hawa wanalala miongoni mwa waliokufa wako nje kule kwenye yale madhehebu yaliyokufa. Wanaelea pamoja nao Mungu analia, “AMUA! Tu pia upumbavu wako” Hapa wanatoa ushawishi wao, muda wao, na pesa zao, tena maisha yao hasa kwa vyama hivi vya mpinga Kristo na wakati wote wanawaza kuwa ni sahihi wanahitaji kutubu, lazima watubu wanahitaji kuwa na badiliko la akili na kugeukia kweli.

Ndiyo, huu ni wakati unapaswa hasa kutubu kuliko wowote. Lakini utafanya hivyo? Utaweza kulirudisha tena Neno? Utaweza tena kumwinua Roho Mtakatifu katika maisha ya watu? Je utamtawaza Yesu kama Mwokozi pekee?

Uamsho, kwa mawazo yangu, haumaanishi kuleta washiriki wapya. Uamsho siyo kundi la waliomgeukia Bwana, ingawa mambo haya yanaenda pamoja na uamsho. Lakini uamsho ni kuamsha kile ulicho nacho tayari kuwafanya waamshwe
(2 Petrol 1:13 – 14)

**Nukuu za kiingereza:**

Mabirika ya vujayo (64-0726E), Aya 74-83
“Israel kule Mistri” (Israel na kanisa sura 1), uk 1/”uwe na hakika na Mungu” Aya 21
“Maswali na majibu” (64-0830E), swali na 395, COD pg, 1161
“Uwepo wa Mungu usiotambulika”, Aya 3/”Kanisa lililodanganywa na ulimwengu”, Aya 73. Nitawezaje kushinda, aya 33/”maswali na majibu” (54-0103M), UMK (COD)uk 66, Aya 48/”kujaribu kumtendea Mungu kazi bila ya Mapenzi yake”(65-1127B), Aya 125 – 130, 155 kumuita Yesu katika kituko (64-0319), Aya 41-50
maswali na majibu 64-0830E swali na 386 utaratibu mwenendo wa kanisa (COD) uk 1158/Muungano usioonekana wa Bibi Arusi, uk 4,8-9/Lile Neno lililonenwa ni mbegu ya Asili, uk 18
“kutambua siku yako na ujumbe wake”, Aya 81-82
Wakati wa kanisa wa laodikia, kitabu cha nyakati uk 356

*jiwe la kiroho la kujengea na 128 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fas : (+49) 72353306.*

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*

*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi kiingereza kiswahili andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*